OFISI YA RAIS TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA

Shule ya Sekondari Mtipe
S.L.P.108
SUMBAWANGA.
14/12/2020

Ndugu: ……

……

Yah: KUCHAGULIWA KUJIUNGA NA SHULE HII.

Ninayo furaha kukufahamisha kuwa umechaguliwa kujiunga na Shule hii katika Kidato cha Kwanza mwaka 2021. Shule itafunguliwa tarehe 11/01/2020. Tarehe ya kuanza kuripoti ni tarehe 04/01/2020 na mwisho wa kuripoti ni tarehe 18/01/2020.

Pamoja na taarifa hii ninapenda kukupongeza na kukukumbusha kwamba nafasi hii uliyopata ni bahati ya pekee ambayo vijana kama wewe wameikosa kwa sababu mbalimbali.
Hivyo ninakukaribisha nikiamini kuwa utaitumia nafasi hii katika kujiendeleza mwenyewe
na Taifa zima.

Yafuatayo ni maagizo ambayo utatakiwa kuyatimiza kabla ya kujiunga na Shule hii.

A: URAIA

Chukua cheti cha Uraia au cha kuzaliwa toka Ofisi ya Wilaya au Mkoa na ufikapo Shuleni umkabidhi Makamu mkuu wa Shule ambaye atakihifadhi katika Jalada lako kwa ukumbusho.

D: A F Y A:

Unatakiwa kuangaliwa Afya yako na Daktari anayetambuliwa na Serikali. Pamoja na barua hii, nimeambatanisha fomu maalum ambayo Daktari huyo atakujazia baada ya kukupima. fomu hii umkabidhi Makamu wa Mkuu wa Shule ufikapo Shuleni.

E: MAPATANO:

Pamoja na barua hii ninaambatanisha fomu ya mapatano ambayo wewe na Mzazi/Mlezi wako mtajaza ili kukubali au kukataa nafasi hii uliyopewa na Taifa na kuahidi kuwa utazifuata sheria za shule ambazo zimeambatanishwa ili uzisome na kuzielewa.

F: SARE ZA SHULE:

Nguo rasmi za Shule (Sare za Shule)

i) **WASICHANA**:-

- Mashati meupe mawili mikono mifupi.
- Sketi mbili (2) moja rangi ya damu ya mzee na nyingine kijani Jeshi
- Hakikisha sketi inayoshonwa izidi usawa wa goti,damu ya mzee yenye malinda na kijani jeshi yenye rinda box na hazibani
- Viatu vya ngozi vyeusi vyenye kamba, visivyo na kisigino kirefu,
- Soksi (Stocking) rangi nyeupe.
- Hijab ya kitambaa cha damu ya mzee au kijani jeshi kwa Wasichana wa kiislamu..
- T-shirt ya rangi ya bluu (itapatikana shuleni).

ii) **<u>WAVULANA</u>**:

- Suruali mbili zenye malinda za rangi ya damu ya mzee na kijani jeshi
- Mashati meupe mawili (2), mikono mifupi.
- Soksi (Stockings) rangi nyeupe.
- Viatu vya ngozi nyeusi vya kamba vyenye visigino vifupi.

-T-Shirt ya rangi ya bluu nyeusi (itapatikana shuleni).

G: <u>NGUO ZA BARIDI:</u>

Wakati wa baridi Mwanafunzi anatakiwa kuvaa sweta za rangi ya kijani jeshi

H: **VIFAA VYA MICHEZO**

- Track suti za rangi ya bluu bahari kwa wasichana wavulana track suti ya rangi nyekundu na bukta nyekundu na fulana nyekundu.
- Raba ya michezo

H: MAHITAJI YA KITAALUMA:

- Counter Book 10 (Daftari kubwa zenye kava gumu quire 2).
- kalamu za wino wa bluu au nyeusi
- kalamu za risasi (penseli)
- Mathematical set/mkebe
- kamusi ya kiingereza
- rimu moja ya karatasi A4

I: VIFAA VYA USAFI

- Fagio aina ya chelewa
- Jembe lenye mpini
- fyekeo au panga
- ndoo moja ujazo wa lita kumi(10)

J: **CHAKULA CHA WANAFUNZI**

Ratiba ya shule huanza saa 1 asubuhi hadi saa 11: 30 jioni, hivyo ni lazima mwanafunzi apate chakula shuleni. Shule ina utaratibu wa kulima mahindi, maharage, alizeti na mbogamboga kwa ajili ya chakula cha wanafunzi. Shughuli hii inasimamiwa na kamati iliyochaguliwa na wazazi wenyewe. Hivyo ni wajibu wa mzazi wa kila mwanafunzi kuhakikisha mtoto anapata chakula shuleni. Shamba hulimwa na wazazi; kupanda, kuweka mbolea na kupalilia hufanywa na wanafunzi. Wazazi hulazimika kuchangia michango kwa ajili ya mbegu, mbolea, mchele, kuni, kusaga mahindi, kukamua mafuta na posho ya wapishi wawili kulingana na jinsi wazazi wenyewe wanavyokubaliana katika vikao. Hivyo ni wajibu wa mzazi kushiriki katika vikao na kutekeleza maazimio ya vikao vya wazazi.

J: <u>M W I S H O:</u>

Ninakutakia maandalizi mema na heri katika masomo yako ya Sekondari.

N:B HAKUNA NAFASI YA KULALA KATIKA BWENI/HOSTERY YA SHULE

SHERIA NA KANUNI ZA SHULE

Shule inaendeshwa kwa mujibu wa sheria ya Elimu namba 25 ya mwaka 1978. Aidha inazingatia miongozo yote inayotolewa na wizara yenye dhamana ya elimu nchini. Mwanafunzi anatakiwa kuzingatia mambo yafuatayo ambayo atafafanuliwa na atapewa nakala yake mara baada ya kuripoti shuleni.

Kwa hiyo kila Mwanafunzi wa Shule hii analazimika kufuata na kutenda yafuatayo.

1. Mwanafunzi haruhusiwi kutumia lugha mbaya wakati wowote kwa Mwanafunzi mwenzake, kwa Walimu na watu wengine.
2. Mwanafunzi lazima awaheshimu Walimu na Wafanyakazi wasio Walimu waliopo shuleni kwani hao ni walezi wake.
3. Mwanafunzi atasimama na kusalimu Mwalimu au mtu yeyote aliyemzidi umri anapopita, anapoingia madarasani na penginepo.
4. Kila Mwanafunzi ni lazima ahudhurie:-
    a) Vipindi kwa muda wote wa masomo na kukaa kimya darasani
    b) Kazi za mikono, shamba na michezo
    c) Baraza la shule, ukaguzi na usafi, kupandisha bendera n.k.
5. Ni marufuku kwa Mwanafunzi kufanya yafuatayo:
    a) Kuvuta sigara au madawa yoyote ya kulevya.
    b) Kufuga makucha na nywele ndefu
    c) Kujinakshi na kupaka wanja na mapambo ya aina yoyote ile
    d) Kuvaa mavazi yasiyo ya heshima.
    e) Kufuga ndevu
    f) Kugombana
    g) Kuharibu mali ya Umma kwa makusudi kama vile: Dawati, kiti, kitabu, n.k.
6. Mwanafunzi haruhusiwi kwenda kwenye majumba ya starehe k.m. vilabuni, nyumba za kulala wageni, n.k.
7. Matatizo yote yanayohusu shule ni lazima yatatuliwe na taratibu zilizowekwa.
   Ni marufuku kwa Mwanafunzi kupeleka malalamiko yake moja kwa moja kwa Mkuu wa Shule au nje ya Shule.
8. Ni marufuku Mwanafunzi kuzurura katika nyumba za walimu au kuonekana bila sababu za msingi

MAKOSA YANAYOWEZA KUSABABISHA KUFUKUZWA SHULE:

1. Wizi
2. Uasherati/Umalaya/ ukuadi
3. Ulevi wa aina yoyote
4. Uvutaji bangi, sigara na dawa za kulevya
5. Kupigana
6. Kuoa au kuolewa
7. Kupata mimba
8. Kutoa mimba
9. Makosa mengine yanayosababishwa na uvunjaji wa kanuni/sheria za Shule.
10. Kuharibu kwa makusudi mali ya Umma
11. Kugomea adhabu.
12. Kuwa na Simu za mkononi.

NB. Ewe mzazi/mlezi wa mwanafunzi tafadhali mwandalie kijana wako mahitaji yote muhimu kwa wakati ili kuepuka usumbufu wa kuchelewa masomo yake na kupoteza nafasi.

Nakutakia utekelezaji mwema

……

STANFORD H. KAMWELA
MKUU WA SHULE

OFISI YA RAIS TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA
SHULE YA SEKONDARI MTIPE

FOMU YA KUANDIKISHWA SHULENI NA HABARI ZA MZAZI/MLEZI WA MWANAFUNZI

A: HABARI ZA MWANAFUNZI

1. Jina kamili kama ilivyoandikishwa kwenye mtihani wa Darasa la saba
   ……..
2. Tarehe ya kuzaliwa: ……
3. Dini: ……..
4. Mahali ulipozaliwa: ……..
5. Shule uliyomalizia Darasa la Saba: ……..

B: HABARI ZA MZAZI/MLEZI

1. Jina kamili ……..
2. Wewe ni Mzazi au Mlezi: ……
   Kama ni mlezi eleza uhusiano wako na Mwanafunzi:
   ……
3. Kazi yako: ……
4. Mahali pa kazi ……(Kama ni Mkulima)
5. Dini ……
6. Wilaya ya Nyumbani ……..
7. Maelezo mafupi kuhusu Afya ya Mwanafunzi:
   ……
   ……

8. Anwani ya Nyumbani: ……..
   ……
   ……
9. Namba ya simu ……

10. Ninathibitisha kwamba taarifa zilizotolewa hapo juu ni kamili na kweli.

……..

SAHIHI YA MZAZI/MLEZI.

OFISI YA RAIS TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA
SHULE YA SEKONDARI MTIPE

FOMU YA KUKUBALI/KUTOKUBALI NAFASI YA KIDATO CHA KWANZA KATIKA SHULE YA SEKONDARI MTIPE MWAKA 2020

1. Mimi …….
   Kidato cha Kwanza katika Shule ya Sekondari Mtipe.

   Nimezisoma kwa makini sana sheria za Shule na ninaahidi kuzifuata. Vilevile nimesoma kwa uangalifu sana maagizo ya kujiunga na Shule na ninaahidi kuwa nitafika na vitu vyote nilivyoagizwa. Natambua kwamba jukumu langu kubwa nikiwa shuleni ni kusoma na kufaulu vizuri katika masomo yote, hivyo kamwe sitokuwa mtoro wa mahudhurio shuleni. Aidha naahidi kutoshiriki katika migomo, fujo na makosa ya jinai. Na endapo nitashiriki hatua kali dhidi yangu zichukuliwe ikiwa ni pamoja na kufukuzwa shule.

…….

SAHIHI YA MWANAFUNZI

UTHIBITISHO WA MZAZI/MLEZI

Mimi …… nikiwa Mzazi/Mlezi wa Mwanafunzi ……. ninakubaliana na ahadi zake na ninaahidi kumsaidia katika kuzitekeleza. Ninaahidi kumtimizia mahitaji yake yote ya Shule kwa wakati unaotakiwa. Aidha naahidi kutoa ushirikiano wa dhati kwa shule ili kufuatilia maendeleo ya mtoto wangu atakapokuwa shuleni.

SAHIHI YA MZAZI/MLEZI

……

PRESIDENT' S OFFICE
REGIONAL ADMINISTRATION AND LOCAL GOVERNMENT

Mtipe Secondary School,
P.O. BOX 108,
SUMBAWANGA.

Date: ……

Medical Officer,
Government Hospital,
……
……

Re: <u>REQUEST FOR MEDICAL EXAMINATION</u>:

Name of student: ……

Please examine the above named as to HIS/HER fitness as indicated below and arrange for necessary treatment if required.

This certificate must be signed by a qualified Medical Officer of a Government Hospital and returned to School by the Student.

<u>MEDICAL CERTIFICATE:</u>

I have examined the above named Student with regard to:-

Skin …… Abdomen: ……
Eyes: …… Stool: ……
Ears: …… Urine: ……
Teeth: …… H.B. Hemoglobin: ……..
Any Disability: ……
……

I consider that:-

1. He/she is in good health, free from infection diseases, worms, bilharzias and is fit to come to school.

2. She is / is NOT pregnant.

…… **……..**
MEDICAL OFFICER **D A T E.**